

MNADA WA KAHAWA YA KAGERA MTANDAONI

Mnada wa Kahawa uliozinduliwa rasmi na Mkuu wa Mkoa wa Kagera Meja Jenerali Charles Mbuge katika ukumbi wa mikutano wa Halmashauri ya Wilaya Bukoba mnamo tarehe 10.06.2022 bado unaendelea ukumbini hapo na kahawa aina ya Robusta na Arabica kutoka katika wilaya mbalimbali za mkoa wa Kagera zinaendelea kuwasilishwa mnadani.

Mnada huu unafanyika mtandaoni na wanunuzi bado wanaalikwa kushiriki kutoka ndani na nje ya Tanzania kwa bei elekezi ya serikali ambayo ni shilingi 1,650/= kwa kilo moja ya kahawa zenye maganda. Aidha mnunuzi mwenye bei nzuri zaidi ya wengine ndiye hushinda na kuuziwa kahawa.

Fuatilia mnada huu katika <http://ots.tmx.co.tz/live/>